



REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

SECOND ASSEMBLY – FOURTH SESSION

THE HANSARD

SPECIAL SITTING

Wednesday, 30th December 2020

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 9.30 a.m.*

[The Speaker (Hon. Kahindi) in the Chair]

PRAYERS

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

SPECIAL SITTING VIDE GAZETTE NOTICE NO. 11256

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Members, this Session has been called pursuant to a Gazette Notice 112556 No. 17 of 2012 County Governments Act; the County Assembly of Kilifi Standing Orders Special Sitting for the County Assembly.

Pursuant to Standing Order No. 26(1) to (4) of the Kilifi County Assembly and the general public that the Assembly shall have a Special Sitting on Wednesday, 30th December 2020, as from 9.30 a.m at the County Assembly of Kilifi premises situated behind Immigration House in Malindi Town.

The main Business to be transacted shall be swearing-in of Dickson Karani Yaa, the newly elected Member of County Assembly representing Dabaso Ward in Kilifi County, Dated 28th December, 2020 and signed by the Speaker. We may now proceed with the ceremony.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ADMINISTRATION OF OATH

(The MCA-Elect for Dabaso Ward Dickson Karani entered the Chamber escorted by Hon. Mramba and Hon. (Ms.) Messo)

The Oath of Office was administered to the following MCA:-

Dickson Karani Yaa

(Applause)

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Members, as a matter of Parliamentary practice, I will now give it to hon. Dickson to make a speech if any, and Serjeants, please help him to switch on the microphone.

The MCA for Dabaso Ward (Hon. Dickson Karani Yaa): Asante sana mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kusema asante kwa watu wote. Nataka kuwashukuru wapiga kura wa Dabaso na wale wote tuliosaidiana kufika mahali ambapo tumefikia leo.

Kwa hiyo mheshimiwa Spika, sitaki kuwa na maneno mengi. Mimi langu tu ningeomba Bunge hili la Kilifi tuwe na ushirikiano mmoja ili kuweza kujenga kwa pamoja hii Kilifi yetu. Asanteni sana. Nitaomba ushirikiano zaidi kwa wote kupitia kwa mheshimiwa Spika, na naamini sote tukishirikiana, mambo mengi yataweza kuwa kwa pamoja. Asante mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Kahindi): I will allow two or three Members to just say something over the same subject.

Hon. Mramba: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa hii nafasi nami kutoa shukrani zangu kwa wana Dabaso katika eneo Bunge la Kilifi Kaskazini. Nina machache ya kuongea; kwanza, tunakuaribisha katika Bunge la Kaunti ya Kilifi, Bw. Dickson Karani mheshimiwa. Kwanza leo, umeingia katika kumbukumbu ya viongozi wa chama cha ODM (Orange Democratic Movement).

Nataka kuwashukuru wale wote waliochangia kuhakikisha kuwa Dickson Karani amefika katika jumba hili, kwanza, watu wa Dabaso, Gavana wetu Amason Jeffah Kingi, na wale wote MCAs (Members of County Assembly) wetu pamoja na Kiongozi wa walio wengi Bungeni. Tulikuja Dabaso kufanya kampeni na tunashukuru Mungu watu wa Dabaso waliyakubali maneno yetu ndio maana Bw. Karani yuko hapa.

La kwanza ni uhakikishe kwamba Januari wanafunzi wanafaa kuenda shuleni. Kuna *Ward Scholarship Fund* kwa hivi sasa Kamati zilikuwa zinachaguliwa upya; ukitoka hapa nakuomba uonane na *Ward Administrator* ama *Sub-County Administrator* uhakikishe Kamati ile ya Dabaso imechaguliwa. Hii ni kwa sababu ile ni *fund* ambayo inasimamiwa, ingawaje sheria ipo lakini wewe kama mwanasiasa lazima ujue Kamati ile imechaguliwa kivi. Pili uhakikishe watu wa Dabaso wanapata haki yao.

Zaidi ya hapo karibu, mengi utajifundisha na najua wewe ni mwanafunzi mzuri sana na kulingana na hata *speech* yako wewe ni mwerevu kwa darasa na nina imani kwamba utasaidia watu wa Dabaso. Kwa hayo mengi au machache, karibu na Mungu akubariki.

Hon. Mwathethe: Thank you Mr. Speaker. I would also like to give some words of congratulations to hon. Karani for his election and also to the people of Dabaso who had faith in him in the election and to my colleagues who went to Dabaso for the campaigns to see that ODM as a Party retains this seat through the by-election.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mr. Speaker it was not easy; it was tough and I also believe that Mr. Karani fought for a long time in the courts to see that justice is served. The election was nullified and a by-election was called and through the by-election we went as a Party. Our purpose was to retain the seat because it was an ODM seat, and for that reason I want to congratulate the people of Dabaso and all the hon. Members.

I know it was not easy during the times of Corona, social distancing and movements, the campaigns were difficult but my fellow Members I wish to thank you for doing a good job for the Party. For that reason I will not have much to say, hon. Karani I have now handed you to hon. Mramba and hon. (Ms.) Philister Messo. They will be your mentors where you need to know something. Mr. Mramba will be near you. I have trust and faith in him he will guide you. If Mr. Mramba is away and you need a lady, hon. (Ms.) Philister will be near you to make you maneuverer a bit, welcome and feel at home. For any other thing the Speaker is there and I am also there and every one of us is there to see that you are comfortable. Thank you.

Hon. Mwamtsi: Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity to give my remarks. First and foremost, I thank God for giving grace to hon. Karani; the grace to be elected in Dabaso. I also want to thank the people of Dabaso and the ODM Party for giving him the ticket, the Rt. Hon. Raila Amollo Odinga, the Governor and all other ODM luminaries that stood by the people of Dabaso to ensure that they got the leader they wanted.

Hon. Karani, you have one year to prove your worth. That one year however short, it is still enough to prove to the people of Dabaso that you are worth them soiling down to elect you. They will not gauge you for the five years some of us have; they will gauge you for the one year you have. With God's grace, 2022 they will re-elect you again. Thank you, Mr. Speaker.

Hon. Pascal: Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity. I would like to first thank the Almighty God for granting victory to hon. Karani and to also thank the people of Dabaso for their decision to vote in hon. Karani.

I have some bit of advice for hon. Karani just like hon. Members have said. You are among those selected to lead the people of Dabaso and looking at the timelines, time is not on your side. I would like to appeal to you that do not let down the people of Dabaso Ward. You have a team that will collaborate and work with you here. The team will give you the support you require to ensure that you serve the people of Dabaso.

Finally, you have joined a club of leadership, and there is a lot you need to do to ensure that you enjoy the dignity of being a leader. Therefore, I would kindly appeal to you that you treat yourself honourably. Thank you.

(Hon. Kenga stood on a Point of Order)

Hon. Kenga: Mr. Speaker, I raise on a Point of Order. The Leader of Majority has mandated that the Member for Dabaso be mentored by hon. Mramba, but Mr. Speaker hon. Mramba has wrongly put on his face mask. As a mentor he may start on a wrong foot. Thank you.

Hon. Ndago: Asante mheshimiwa Spika. Pia mimi nataka kuchukua nafasi hii kwanza nimpongeze mheshimiwa Dickson Karani pia vile vile niwashukuru watu wa Wadi ya Dabaso kwa kuonyesha ukomavu wa kisiasa. Tukiangalia mawimbi tuliyoyapitia Dabaso yalikuwa si mawimbi madogo, lakini kwa sababu ya heshima ya watu wa Dabaso kuonyesha kwamba walikuwa wamechoka na walitaka mageuzi, wakatupatia Dickson Karani.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Langu tu mimi ni kukusihi, kuna mengi ambayo tumewaahidi watu wa Dabaso, na hapa leo umeapishwa rasmi kama mwakilishi wa Wadi ya Dabaso kisheria. Ni wajibu wako kuonyesha utendakazi, ule ushirikiano ambao ulitonyesha sisi kule nyanjani uonekane hapa kwa hili Bunge. Na pia vile vile ushirikiano huo upeleke kule Dabaso kwa wananchi; hivi leo wewe umechaguliwa si Diwani wa ODM peke yake, ni Diwani wa kila mtu pale Dabaso...

(Hon. Pascal stood on a Point of Order)

Hon. Pascal: Thank you Mr. Speaker. I would like to either correct or inform the hon. Member that the title *Diwani* no longer exists; we have hon. MCA that exists. Thank you very much Mr. Speaker.

Hon. Ndago: Asante sana mhesimiwa Pascal Thuva. Nakuheshimu sana kama kiongozi na pia nakuheshimu kama mkubwa wetu hapa ni ulimi tu umeteleza. Nataka niamini ya kwamba, mheshimiwa huyu wa Dabaso atawakilisha kila mtu bila kubagua, chama ama rangi wala dini. Mheshimiwa Dickson Karani umeingia kwa wakati kidogo sana, lakini naamini ndani ya Bunge hili na uongozi ulio hapa utapata mwelekeo mwema na utapata usaidizi wa kutosha. Langu lengine ambalo ningependa kusihii uongozi wa Bunge kupitia kiongozi wa walio wengi, mchukue wakati wenu mzuri na mapema kuhakisha kwamba ndugu yetu Dickson Karani amewekwa katika zile Kamati ambazo zinalingana na utendakazi wake.

Nikimalizia, najua haiko kwa Biashara ya leo, lakini mheshimiwa Spika kwa heshima yako ningependa kutoa rambi rambi zangu kwa watu wa Kaloleni kwa kuondokewa na ndugu yetu, kiongozi wa kisiasa mheshimiwa Gunga Mwinga. Mwenyezi Mungu akailaze roho yake mahali pema peponi, tuweni pole sote na Mwenyezi Mungu azidi kutulinda na tuwe na mwaka mpya wenye fanaka na baraka nyingi.

Hon. Ziro: Asante mheshimiwa Spika kwa nafasi hii nami niweze kumpongeza ndugu yangu mheshimiwa Karani kwa nafasi hii ambayo watu wa Dabaso wameweza kumpatia ili aweze kuja katika Bunge hili. Mimi kama Askofu, ningependa kupeana wasia kidogo, na nashukuru Mungu watu wa Dabaso wako hapa.

Wakati wana wa Israeli walipotoka Misri, walikuwa wameahidiwa kuingia katika mji wa Canaan. Walitolewa na Musa na nataka kumchukua ndugu yangu Karani kama Musa, na watu wa Dabaso ni kama wale waliotoka Misri, kabla hawajafika katika ile nchi ya ahadi, walipofika pale jangwani kulikua na...

(Hon. Mramba stood on a Point of Order)

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Mramba, let us hear the sermon. You are protected hon. Ziro.

Hon. Ziro: Asante sana mheshimiwa Spika. Mungu akubarika maanake naona kuna kiti cha Mungu ndani yako.

Wakati wana wa Israeli walipofika katikati ya jangwa kukaanza kuonekana kwamba kuna mawimbi na matatizo tofauti ambayo walianza kumlilia Musa mpaka Musa akawakimbia na kuenda kumlilia Mungu mlimani.

Langu ni kusema ya kwamba, mheshimiwa Karani amechaguliwa wakati ambapo siasa ya 2022 imeanza. Hawa watu wa Dabaso, sisi kama Bunge tuko tayari kumsaidia mheshimiwa Karani ili aweze kuwa msaada kwa watu wa Dabaso. Wasiwasi wangu ni kwamba watu wa Dabaso wamuunge mkono maanake anaweza kuwa na udhaifu wake. Hilo ndilo ombi langu kwa

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

watu wa Dabaso hasa wale walio hapa maanake naona viongozi tofauti wamekuja kushuhudia kuapishwa kwa Musa wao.

Mheshimiwa Spika, mimi sina mengi. Iikua tu ni kupeana wasia wa Kibibilia na wa kidini kama askofu ili kesho Mungu asije akanilaumu kwani nilikuwa hapa na sikupeana wasia. Asante mheshimiwa Spika.

Hon. Baya: Asante mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii ili pia mimi nikaungane na wenzangu tuweze kumpongeza mheshimiwa Dickson Karani kwa kupata nafasi hii. Pia mimi kama jirani yako, nakupongeza sana kwa ushindi huu uliopata lakini wengi wametangulia kunena changamoto zilizo mbele yako, ikiwa moja yapo ni mda na matarajio.

Mimi lile ambalo ningependa kukupa kama wasia wangu ni kwamba usisikize ya watu maanake usitazamie kila mahali utakapoingia utaambiwa ni wewe tu. Kwengine utapata changamoto lakini muhimu ni yale mambo uliyoyaongea pale ya kwamba uweze kutii sheria na uweze kuongoza watu wa Dabaso kwa mujibu wa sheria. Kwa hayo mengi au machache nasema shukrani sana. Karibu sana na kama unataka wasia ama ushauri wowote unakaribishwa, mimi si kitambo sana lakini kufikia sasa naweza sema nitarudi tena. Asante.

Hon. Gogo: Asante mheshimiwa Spika kwa nafasii hii. Ningependa kutoa ushauri mchache kwa ndugu yetu mheshimiwa Dickson Karani. Kwa ajili ya wale wageni ambao tuko nao leo katika Bunge hili, kwa majina ni mheshimiwa Victor Gogo. Mimi ni mchaguliwa wa wodi ambayo inaitwa Mtepeni upande wa Kilifi South. Mimi ni mfuasi sugu sana wa Askofu Ziro ambaye ni mheshimiwa wa Bunge hili. Nimekuwa nikitembea katika kanisa lake na nimejifundisha mambo mengi katika mahubiri yake. Siku moja alihubiri mambo kuhusi Daudi, ya kwamba Daudi alipokuwa hajapakwa mafuta yani kuchaguliwa kuwa kiongozi rasmi aliishi na furaha sana. Lakini siku ile alipotawazwa na kupakwa mafuta kama kiongozi hapo ndipo vita ndio vilianza.

Kwa hivyo, nataka kumshauri rafiki yangu Dickson Karani kwa sababu leo ametawazwa kuwa MCA wa Dabaso hata wale ambao walikuwa marafiki zake wengi waliokuwa wakimfanyia kampeni wao ndio watakaokuwa maadui wake wa kwanza lakini nataka nimpatie moyo kwamba yote inawezekana akiwa na ile imani ilimfanya kupigania haki yake mpaka uchaguzi ukarudiwa tena katika wodi hiyo ya Dabaso.

Na sababu tuko na wafuasi wengi wa wadi hiyo ya Dabaso, nataka niwapatie ushauri wananchi wa Dabaso ya kwamba maendeleo ya Dabaso hayatakuja kwa mwaka mmoja na nusu ambao umebakia. Ni kazi ngumu mheshimiwa Karani (Dickson) kubadilisha Dabaso kwa mwaka mmoja na nusu, mpatieni wakati mheshimiwa, msimpatie presha nyingi sana ya kwamba hata ashindwe kufanya kazi. Mpatieni nafasi kijana wenu afanye kazi mda huu mchache na pia nitakuwa mtu wa kwanza kulingana na vile nilivyomuona kwamba anaweza kupigania haki kwamba pia 2022 mmpatie wakati mzuri awafanyie kazi. Kwa hayo mengi na machache, ninamkaribisha Dickson Karani katika nyanja hii ya uongozi na kwa sababu ni kijana wa kanisani, Mwenyezi Mungu atampatia hekima na maarifa kuwafanyia kazi wananchi wa Dabaso. Asante.

Hon. Shaban: Asante mheshimiwa Spika. Mimi pia nataka niungane na wajumbe wenzangu kusema karibu mheshimiwa Dickson Karani katika Bunge letu la Kilifi na pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kufanya kampeini ambayo iko sawa hatimaye ukaweza kuibuka mshindi.

Mheshimiwa Dickson Karani, sisi tunafuraha kwa sababu hiki kiti kilikuwa ni cha ODM na kimerudi nyumbani. Kwa hivyo, karibu sana na watu wa Dabaso tunashukuru kwa kutuletea kijana ambaye atafanya kazi katika miaka iliyobakia ili tuhakikishe kwamba Dabaso imepiga

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

hatua mbele tukijaribu kuokoa ule mwaka mzima ambao tuliupoteza ndio tukawa na huu uchaguzi.

Mwisho kabisa, nataka niungane na mheshimiwa Sammy Ndago kupatiana rambirambi zangu kwa kuondokewa na mheshimiwa Gunga Mwinga kule Kaloleni. Ni msiba ambao sisi kama watu wa Kaloleni na Rabai tunahuzunika sana kupoteza kiongozi wa tajriba kama ile lakini wacha tuombe Mwenyezi Mungu aweze kuifariji familia katika wakati huu mgumu wa maombolezi. Asanteni na Mungu atubariki tunapokaribia mwaka mpya wa 2021. Tukiomba Mwenyezi Mungu kwamba mwaka unaokuja hautakua na changamoto kama huu ambao tunaupatia kwaheri. Asante mheshimiwa Spika.

Hon. Reuben: Asante sana mheshimiwa Spika kwa fursa hii. Pia mimi vile vile ningependa kuungana na wale waliotanguliza semi zao kumpongeza mheshimiwa Dickson Karani. Saa hii wewe uko na kofia ya uheshimiwa kweli kweli katika jiji zima la Dabaso. Kawaida hapa katika hili Bunge mimi nilikuwa nashikilia kile kigongo cha kitinda mimba lakini saa hii nimekutweka wewe; kimenitoka nimeenda sehemu nyengine. Ndugu yangu, mimi nataka kushukuru wananchi wa Dabaso kwa juhudi zenu; zile mbio hazikuwa rahisi. Nilikuwa kule mimi niliona vile vumbi lilikuwa linatimuka si rahisi lakini mlizitatiti kuhakikisha kuwa ndugu yangu Karani anaibuka mshindi katika kile kinyang'anyiro cha Dabaso. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Vile vile ningependa kumshukuru mstahiki Gavana Amason Jeffah Kingi kwa bidii zake. Alijizatiti kwa hali na mali; kwa maneno na kila kitu kile Mwenyezi Mungu ambariki. Nawashukuru pia waheshimiwa tulioungana pamoja katika Bunge hili la Kilifi ili kuhakikisha kwamba mheshimiwa Karani amechaguliwa kuwa MCA wa Dabaso. Ushauri wangu ningependa kuuelekeza kwanza kwa wenyeji wa Dabaso. Hii nafasi ambayo mmempatia, najua mlikuwa na mapenzi ya kibinafsi yaliokuwa ndani yenu ambayo hayo tusipoyachunga kuapishwa kwake huyu kunaweza kuwa mwanzo wa vita baina yake na nyinyi. Kuna wengine wanaweza kuwa wana matarajio ya kuwa akichaguliwa huyu nataka niwe meneja wa hiyo ofisi na kuna wengine mko kama watano. Yeye akichukua mmoja, wengine itakuwa ni vita. Hilo ni onyo ninawapa wananchi wa Dabaso. Mwenzako ukiona amechaguliwa hapa tafadhali uwe radhi kwa sababu nyote ni wananchi wa Dabaso. Msimuwekee vita huyu.

Pili, ndugu yangu ninaongea haya kwa sababu mimi nilichaguliwa juzi na ninayaona kule. Kipindi hiki ni kidogo na ulichaguliwa katika hali ya kura elfu mbili (2,000) na utarushiwa mawe mengi tena sana, lakini mawe yale usiyaokote ukawaregeshea maadui. Ukirushiwa mawe yaokote ujenge msingi wa Dabaso...

(Applause)

Wapinzani watakuja na mbinu tofauti tofauti huku na huku lakini wewe yaepuke hayo maneno; fanyia kile kinapasa wananchi wa Dabaso. Mwisho wa siku wataangalia yale ambayo umeyafanya hatimaye 2022 utarudi hapa tuwe pamoja tena katika hili Bunge.

Mwisho, napenda kuungana na mheshimiwa Ndago juu ya msiba ambao ulitupata japo hauko katika ratiba ya leo. Mheshimiwa Gunga Mwinga urafiki wake mimi na yeye ni wa kipekee japo yeye yuko mbali maanake mimi niko Ganda yeye yuko Kaloleni lakini mimi nilipoingia siasa hapa baada ya kutoka chuo kikuu aliyeniingiza kwenye siasa ni mheshimiwa Gunga Mwinga. Yeye ni babangu wa kisiasa; wakati huo tulikuwa tuko katika *by-election* ya hapa Malindi. Mwezi wa tatu tarehe saba 2016 mimi nikawa nagombania kiti na tikiti ya Kadu Asili akaniingiza katika siasa. Yeye ndie alikuwa *steering* yangu. Akaniingiza katika siasa kwa

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

hivyo watu wamepoteza kweli lakini mimi kibinafsi nimepoteza babangu wa kisiasa. Nasema tuweni pole sana wananchi wa Kilifi. Mwisho mheshimiwa Dickson Karani karibu Bungeni.

Hon. Kenga: Asante sana mheshimiwa Spika kwa nafasi uliyonipa. Nimeomba hii nafasi ili kwanza kabisa niweze kumpongeza mheshimiwa Dickson Karani Yaa kwa sababu ya ushindi ambao aliweza kuupata wakati alipoenda katika nafasi ya ugombezi. Leo tunapoendelea kusherehekea mheshimiwa Spika, niseme kwamba hatma ya sherehe ile ya ushindi wananchi wa Dabaso wamefika ili kushuhudia ukiapishwa rasmi kuwa mwakilishi wa wadi ya Dabaso. Basi ili wananchi wapate nafasi ya kuendelea kusherehekea ni lazima matarajio yao, malengo ambayo walikuwa nayo ndio waweze kukuchagua upate nafasi ya kuyatekeleza.

Naamini watu wa Dabaso wanaelewa kikamilifu kwamba yale ambayo ni matarajio na malengo ni lazima yaende kwa mujibu wa sheria kama ulivyoapa. Hivyo basi, nataka niulize kwamba utakuwa makini ili uweze kuwatekelezea wajibu wako kama mwakilishi wa wadi majukumu yako uyatekeleze kwa uaminifu ukizingatia sheria lakini zaidi wananchi wapate nafasi ya kushuhudia maendeleo katika wadi ya Dabaso kupitia kwa uongozi wako. Itahitaji ushirikiano wa dhata, uwe karibu na wananchi na tupate nafasi ya kusonga mbele kama ulivyosema kwamba ni jukumu letu kwa ushirikiano tuweze kujenga Kilifi yetu, Dabaso ikiwemo ndani ya Kilifi.

Mheshimiwa Spika, hata sikutaka labda pengine nizingumze lakini nikaangalia kwamba makaribisho yetu hayatakamilika kama sauti ya viongozi wa jinsia ya kike haitasikika kumkaribisha ndugu yetu mheshimiwa Dickson Karani. Nimeangalia mnenaji wa kwanza; kiongozi wa walio wengi Bungeni, tukaenda mpaka mahali tumefika, zaidi ya viongozi kumi tumezungumza lakini hakuna sauti ya mama ambayo imesikika na sidhani kama tutakuwa tumefanyia haki mheshimiwa Dickson Karani kwa kumnyima ama kukosa nafasi kina mama wa Bunge hili waheshimiwa kuweza kumkaribisha. Kwa hivyo, mheshimiwa Spika, ningomba tuweze kuskia sauti ya viongozi wetu wakimkaribisha ndugu yetu mheshimiwa Dickson Karani. Asante sana.

Hon. (Ms.) Philister: Thank you Mr. Speaker. DS (Deputy Speaker) for your information, I applied a long time ago so do not worry; we were just waiting for our time. Hon. Karani, I congratulate you plus Dabaso people. I have simple advice to you; you tried with KADU Asili but you could not capture that seat, but this time you decided to join ODM and you have captured that seat. So make sure you respect your Party and Party leader because most people so long as they get that ticket and within no time they change their minds because of money.

So I advise you to respect your Party leader, the Leader of Majority in the House and all Members in this House. So come 2022, it will be something so easy for you to capture it and when working, please don't mind about ODM, work for all Dabaso people; those who voted for you and against you. You are now their leader. Thank you so much Mr. Speaker, Sir.

Hon. Mwayaa: Asante mheshimiwa Spika. Kama *senior* na kama Kiranja wa Bunge nachukua fursa hii pia nimkaribishe ndugu yetu Karani kwa ushindi ambao aliupata kule Dabaso na pia vile vile niwashukuru watu wa Dabaso kwa kufanya siku ya leo kuwa vile ilivyo. Nitaongea tu mawaidha kidogo kwa sababu ya ule *senior* niko nao; nikisema hivyo ni kwamba siasa tulianza mbali kutoka 2002 na mpaka sasa tuko bado kwenye siasa. Ushauri kwa watu wangu wa Dabaso, upishi wa pilau hauishii kubandika sufuria na ule moto mmoja ambao mtakuwa mumeubandika. Upishi wa pilau unaendelea mpaka muweke makaa ya juu na hapo ndio pilau itakuwa inaendelea kuiva. Leo hii tumemuapisha Dickson Karani, mkasema ameapishwa na mkikaa mbali mtakuwa mnapika pilau na moto mmoja na huenda ikawa si pilau

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ikawa ni sima na malengo yenu kama ni kula pilau basi sufuria mumeibandika leo, mnaendelea nayo mpaka muweke makaa ya juu ndio iive. Huu msemu uchukulieni kwa uzito. Leo hii mumemuapisha Karani, vigelegele viko na mtasema ni kiongozi muende mkakae bila kumshauri wala kukaa naye karibu na kuona barabara mtakayoshika ni barabara gani. Bila makaa ya juu hamtakula pilau ndugu zangu wa Dabaso na pilau ni mpaka iwe na makaa ya juu.

Nikirudi kwa ndugu yangu, umeapa hapa na hapa ndani kama uko na mke hakuingii mke wako; pengine amekuangalia kwa *gallery* ukiapa. Ukifika kule uliyaapa hapa mregeshee afunge milango akaribishe watu wa Dabaso. Akiona watu wa Dabaso wanakuja akifunga milango anakufungia kazi. Muache milango wazi, afagie ile *compound* kwa ajili ya kukaribisha wageni. Ndugu yangu Karani, kama ulikuwa ukilala mpaka saa mbili saa hii sahu. Utakuwa ukibishiwa kuanzia saa kumi na mbili hadi saa mbili, na saa kumi na mbili, saa moja, saa mbili. Kwa hivyo, ongeza viti na ukaribishe wageni ndani. Pia, hata kama vijiko vimepungua ulete kwa sababu wengine watakuja bila hata kupata kifungua kinywa na watakaokuja kwa kiongozi wao ni wewe. Hayo tumeyaona maanake tumekaa huko kutoka 2002 mpaka saa hii ndio mawaidha hayo tunakupatia. Uwe mkaribifu wa watu.

Uongozi si rahisi. Sisi tumezoea na nitayaongea hapa. Umeletwa hapa ukifika kule huna maana tayari; uyasikie hayo. Saa hii uko na maana hata umeletwa na wengi, hata wale *campaigners* wako wataenda watakuchenga hata pengine baada ya wiki mbili. Sisi tuliyaona. Nilipigwa na jamaa mahali kwa mkutano na tulivyorudi mwenzangu akarudi nyuma. Hayo yachukue kwa uzito, uwe na ujasiri na ufanyie kazi watu wa Dabaso na sisi kama wenzako hapa Bungeni ukituuliza ushauri tutakuambia ili Dabaso iende sawa sawa na matarajio yao. Asanteni watu wa Dabaso. Asante ndugu Karani kwa kuletwa kwa Bunge hili. Tutakuunga mkono mia kwa mia na wakati ukitaka ushauri tutakupatia.

Vile vile mheshimiwa Spika nichukue fursa hii nami nitoe rambi rambi zangu kwa rafiki yetu mkubwa wakili wa kwanza pale Kaloleni. Tumepoteza wakili ambaye alikuwa ni mpenda watu, tumepoteza kiongozi wa siasa ambaye alikuwa ni shupavu na kilikuwa ni kifo cha ghafla. Wacha nitoe rambi rambi zangu kwa familia yake ifarijike. Mungu ailaze roho yake peponi na hayo itabidi tukubali maanake ni mambo ya Mungu. Asante mheshimiwa na tubarikiwe sote.

Hon. (Ms.) Loice: Asante sana mheshimiwa Spika kwa kupata hii nafasi. Niseme pongezi sana kwa mheshimiwa Dickson Karani ambaye ni ndugu yangu. Tulijuana wakati wa kampeni zake, tukahudhuria kampeni ya maeneo ya Mkangagani. Niwapongeze sana wakaazi wa wadi ya Dabaso kwa kumchagua kijana mpole sana. Tulikuwa naye mwenye alikuwa lakini alikuwa machachari kidogo. Lakini huyu ambaye mumetuletea na akaapishwa nafikiri kwa mda huo mchache ambao unaendelea hapa anaweza kufanya mambo mengi sana mkishirikiana naye vizuri mheshimiwa Dickson Karani nafikiri wale ambao tulikuwa siku ile tulikuapisha. Ukikumbuka hiyo siku na tukakuahidi kwamba utaingia katika Bunge hili na nafikiri umeshuhudia kwamba leo uko hapa karibu sana lakini pale Mkangagani kuna mambo tuliahidi. Juzi nilipata simu kutoka huko wakati ulipotangazwa mshindi; wananchi wanasema tulimpigia Karani sasa tunasubiri ahadi zenu kama mlivyoahidi. Tutashirikiana kuhakikisha tumetimiza hizo ahadi ili tuwe waaminifu kwa wananchi. Kwa hayo machache asante sana, na wanadabaso wadi ambao mko hapa leo kushuhudia kuapishwa kwa Mheshimiwa wenu nawaomba mkashirikiane vizuri naye katika kutimiza malengo ya wadi yenu. Karibu katika Bunge na Mungu akubariki.

Hon. Peru: Thank you Mr. Speaker for granting me this opportunity to welcome hon. Dickson Karani to the County Assembly of Kilifi. I want to congratulate the people of Dabaso for tirelessly working hard to ensure that Karani is in this Assembly. My advice to my brother is

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

in this House ODM is the Majority Party; you will need team work with other Members so that when you bring a Motion concerning the people of Dabaso here, you will have the support of the Members.

As an ODM Member having experience of roughly three years, ODM is a solid family and it had depicted itself to you through the campaigns we did against Changawa. In politics there is no enemy. All there is is interest; just ensure your interests are synchronized with the Party and the people of Dabaso. You have one year; most Members are engaging on gear one of campaign period of 2022 elections. Do not sit back. Work for the people of Dabaso and I am sure they will give you another opportunity.

Hon. Matsaki: Asante Bw. Spika kwa kunipa nafasi hii ili kumkaribisha Bw. Karani. Mengi yamezungumuzwa. Nataka kusema kitu kimoja na sitasema na Dickson Karani kwa sababu yeye yuko na muda mfupi sana. Kwa wale ambao wako hapo juu naitwa mheshimiwa Valentine Matsaki Mwamanga. Mimi ni kiongozi wa wachache katika Bunge hili. Watu wa Kadu Asili tumekuwa na shida. Tunawabeba watu wengi mwisho wana...sitasema wanunuliwa lakini wanachukuliwa kwenda kule ambako wanafikiria watasaidika. Hata mheshimiwa Reuben, ukiangalia simu yangu kuna pesa nyingi nilituma kwa kesi yake lakini dakika za mwisho akachotwa; tusidharau vyama vyetu tuko hapa tukiwa kwa hicho chama.

Nataka kuongea na wananchi wa Dabaso. Mlimchangua na kumleta hapa, sasa muda uliosalia ni mchache sana kwa hivyo msitarajie mengi. Nilikuwa ninashauriana na wenzangu katika Kamati ya kuwapa waheshimiwa mikopo kama anaweza kupata gari, lakini msimuone na gari mkaanza kuwa adui. Mtasema alienda hana kitu sasa ana gari. Naomba mmchukulie kama ndugu yenu. Mkitaka maendeleo mengi ni ifikapo 2022 mmrudishe kwa sababu kwa mda uliobaki ni kidogo hakuna maendeleo mengi anaweza fanya kwa sasa.

Nataka kuunga mkono kile Mwenyekiti wa Kamati ya *Scholarship* mheshimiwa Mramba amemwambia kuhusu mambo ya Kamati, kwa sababu najua pesa ziko. Hizo pesa utapewa uangalie utafanya nini nazo wewe mwenyewe. Kuhusiana na maendeleo, sijui kama katika hizi pesa zetu shilingi milioni 25 kuna zenye zilibaki kwa sababu kwa wakati huo kulikuwa na Changawa. Siasa nzuri ni uwe karibu na watu wako na kuwa makini wasikiza mahitaji yao.

Miezi miwili baada ya mheshimiwa Reuben kuchangulia alikuwa karibu kupigwa na wananchi wake katika *stage* moja hapo kwake kwa sababu walimuona na gari. Hii siasa ni ngumu haya sio maeneo ya mzaha ni mambo ambayo tumepitia kama ulivyosikia mmoja amesema yeye ni *senior* aliingia 2002 na sisi tuliingia toka miaka ya tisini na bado tuko katika siasa. Kaa karibu na watu wako, uko nacho huna kaa na wao; ukiwahepa kwa sababu unasema huna kitu hapo utanza kuleta shida. Ukiwahepa, hiyo 2022 utaiona paa sio ajabu ukarudi Kadu Asili.

COMMUNICATIONS FROM THE CHAIR

MOMENT OF SILENCE IN MEMORY OF THE LATE HON. GUNGA MWINGA

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Members, before we take our adjournment, I also want to stand with hon. Ndago to eulogize the late Gunga. He is a colleague; he is somebody who has also mentored me in the legal profession and being the leader of this sitting, I would request that we all stand up and observe a minute of silence in his remembrance.

(Members stood for a moment of silence)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

PHOTO SESSION WITH THE NEWLY SWORN-IN HON. MEMBER

Hon. Members, I am informed that there will be a photo session of the newly sworn-in Member outside there.

ADJOURNMENT

In the absence of any other business on the Order Paper, the House goes back on recess until the date that we will be resuming back. Thank you.

The House rose at 11:00 a.m.